**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA TANZANIA**

# TAARIFA KWA UMMA

Dodoma, 21 Agosti 2024

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Franklin Jasson Rwezimula, ameipongeza Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania (LRCT) kwa hatua yake ya kuzindua Law Reformer Journal, jarida la kitaaluma litakalojikita katika masuala ya utafiti, uchambuzi na mapendekezo ya maboresho ya sheria nchini.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa jarida hilo, Dkt. Rwezimula alisema kuwa hatua hiyo ni muhimu katika kuimarisha mfumo wa utoaji wa taarifa, tafiti na maarifa kuhusu masuala ya kisheria, hasa kwa wataalamu wa sheria, wanasayansi, watunga sera na wananchi kwa ujumla.

"Uzinduzi wa Law Reformer Journal ni hatua kubwa inayochangia katika kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala ya kisheria na kuhamasisha mijadala yenye tija kuhusu maboresho ya sheria nchini. Jarida hili litakuwa jukwaa muhimu la kubadilishana mawazo na uzoefu wa kitaalamu," alisema Dkt. Rwezimula.

Aidha, Dkt. Rwezimula aliipongeza Tume kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuendana na mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia yanayoathiri mfumo wa sheria. Alisisitiza kuwa Wizara ya Katiba na Sheria itaendelea kushirikiana na Tume hiyo katika kuhakikisha tafiti na mapendekezo yanayotolewa kupitia Law Reformer Journal yanatumika katika kuboresha sera na sheria za nchi.

Kwa upande wake, viongozi wa Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania wamesema kuwa Law Reformer Journal itachapishwa mara kwa mara na itapatikana kwa njia ya kidijitali na nakala ngumu, ili kuhakikisha inawafikia wadau wengi zaidi ndani na nje ya nchi.

**Bashiri. S. Juma**

**Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - LRCT**

*Chuo Kikuu cha Dodoma,Barabara ya Mkalama,Jengo la Taaluma Na.1,S.L.P. 1718, Dodoma.*
*Tovuti: www.lrct@lrct.go.tz; Barua pepe: lrct@lrct.go.tz; Simu: +255734 356685/6*